

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Apongezwa kwa Kuishauri Vizuri Serikali Masuala ya Sheria

Na Mwandishi Wetu

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari amekutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Kamati ya Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilmali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) Mhe. Balozi Wilson K. Masilingi, leo Aprili 14, 2026 katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bungeni, Jijini Dodoma.

Balozi Masilingi ambaye aliteuliwa

na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI Januari 29, 2026 amemtembelea Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kujitambulisha na kumpongeza kwa kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya kuishauri Serikali katika masuala ya kisheria nchini.

Aidha, katika Kikao hicho, Viongozi

hao wamejadiliana namna bora ya kuimarisha zaidi Ushirikiano uliopo baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na TEITI.

Katika ziara hiyo Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI aliambatana na Katibu Mtendaji wa TEITI Bi. Mariam Mgaya.